

HAKIELIMU 2017 – 2021

MPANGO MKAKATI WA HAKIELIMU (MUHTASARI)


ACHIEVING OUR COUNTRY
Political Disagreement
Toward a Theory of Governance
CIVIC EDUCATION AND CULTURE
Mediated Politics
HOWARD ZINN
A POWER
Everyday Politics
Civic Engagement, Digital Networks, and Political Reform in Africa
Decentralization in Uganda
THINK TANK TRADITIONS
Barry
The Captive Public
BRUNVAND GROBING
BRAINWASHED
Tom Harris
IT GOVERNANCE
AMOS TUTUOLA
SOPHIA MUSTA
THINGS FALL APART
TO KILL A Mockingbird
FARM CITY



YALIYOMO

DONDOO MUHIMU KUHUSU HAKIELIMU 2

- Dira 2
- Dhamira 2

1.0 HISTORIA YA ELIMU TANZANIA 4

1.1 Mageuzi kwenye elimu baada ya uhuru 4

1.2 Kushughulikia ubaguzi wa kidini, rangi na kimapato 4

1.3 Mahitaji ya wafanyakazi wa kiafrika (Afrikanaizesheni) 4

1.4 Maendeleo miaka ya hivi karibuni 5

1.5 Juhudi za Serikali na Mafanikio 5

1.6 Changamoto za Elimu 6

2.0 TUNATAKA KUFANYA NINI: MAENEO TUNAYOLENGA KATIKA MPANGO MKAKATI 2017-21 7

2.1 Kushawishi mabadiliko ya sera na utekelezaji wake 7

2.2 Kukuza ushiriki wa wananchi na kujishughulisha 9

2.3 Kukuza uwazi na uwajibikaji 11

3.0 TUNAFANYAJE KAZI? 12

Dondoo muhimu kuhusu HakiElimu

HakiElimu ilianzishwa mwaka 2001 na kundi la Watanzania 13 ambao waliweka nia thabiti na dhamira ya dhati na ya muda mrefu kuleta mabadiliko kwenye elimu ya umma kwa watoto wote.

Dira

Kuwa na Tanzania yenye uwazi, haki na demokrasia ambapo watu wote wanafurahia haki ya kupata elimu bora inayokuza usawa, ubunifu na kufikiri kiyakinifu.

Dhamira

Kuwawezesha watu kubadilisha elimu, ndani na nje ya shule; kushawishi utungaji wa sera na utekelezaji wenye ufanisi; kuchochea mijadala bunifu ya umma na mabadiliko ya kijamii; kufanya tafiti, uchambuzi wa sera na utetezi na kushirikiana na wadau ili kukuza ushiriki wa wananchi, uwajibikaji, uwazi na haki za kijamii.





1.0

HISTORIA YA ELIMU TANZANIA

Mwenendo wa hivi karibuni wa bajeti ya elimu unaonesha kuwa bajeti ya elimu ya Tanzania imeendelea kubaki kiwango cha 21% ya bajeti ya taifa. Hata hivyo, mgawo wa sekta ya elimu kwenye bajeti ikiwa ni pamoja na kulipa madeni ya taifa imebakia katika wastani 17%, ikimaanisha kuwa kwa miaka kadhaa hakujawa na ongezeko kwenye eneo hili ikilinganishwa na bajeti ya taifa.

1.1 Mageuzi kwenye elimu baada ya uhuru

Mwalimu Julius Nyerere, Rais wa kwanza wa Tanzania alikuwa kiongozi mwenye maono ambaye alikuwa na wazo lililokuwa wazi kabisa kuhusu aina ya jamii aliyotaka kuijenga nchini Tanzania. Chini ya uongozi wake, mwaka 1967 Tanzania ilichukua rasmi Sera ya Ujamaa kama falsafa elekezi kwenye jitihada zake za kujiletea maendeleo. Lengo la serikali iliyoundwa baada ya ukoloni lilikuwa ni kujenga umoja, usawa na kuimarisha ushiriki wa wananchi kwenye harakati za kuleta maendeleo katika maeneo yao na taifa

kwa ujumla. Mapema tu baada ya kupata uhuru mwanzoni mwa miaka ya 1960, mfumo wa elimu pia ulianza kufanyiwa mageuzi hatua kwa hatua ili kuendana na malengo haya mapya ya serikali.

1.2 Kushughulikia ubaguzi wa kidini, rangi na kimapato

Kabla ya uhuru wa Tanzania Bara mwaka 1961, vyombo mbalimbali vya vilikuwa vikitoa elimu, kwa kuzingatia misingi ya rangi, dini na hali ya kiuchumi ya wananchi. Lakini mwaka 1962, Sheria ya Elimu ilipitishwa, sheria hii ilipiga marufuku utoaji elimu kibaguzi kwa kuzingatia rangi, udini na hali za kiuchumi. Ada na karo za shule zilifutwa mwaka 1963, na hivyo tatizo la kihistoria la watoto wa kiafrika kutengwa na kubaguliwa kwenye elimu likawa limeshughulikiwa.

1.3 Mahitaji ya wafanyakazi wa kiafrika (Afrikanaizesheni)

Baada ya uhuru, Serikali iliona kuna haya kwa Watanzania kuchukua nafasi za kazi ambazo zilikuwa zinafanywa na Waingereza hasa baada ya wafanyakazi wengi wazungu kuamua kuondoka nchini baada ya uhuru. Serikali iliamua kupanua elimu ya sekondari na elimu ya ufundi ili kukidhi mahitaji hayo ya wafanyakazi. Taifa likaanzisha Sera ya Elimu ya Kujitegemea (EK) ambayo iliwaandaa wanafunzi kwa ajili ya jamii ya kijamaa.

1.4 Maendeleo miaka ya hivi karibuni

Tangu miaka ya 1990 sera za Serikali, zimekuwa zikiongozwa na ajenda za kiliberali za soko huria chini ya uongozi na msaada wa Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Ulimwenguni (IMF). Baada ya EK,



sera muhimu zaidi ya elimu iliyotungwa ni Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995, sera hii iliongoza sekta ya elimu kuanzia katikati ya miaka ya 1990 kwa kipindi cha muongo mmoja na nusu. Malengo ya elimu yalibadilika kutoka kuandaa wanafunzi kuwa wazalishaji kwenye uchumi kijamaa hadi kuwaandaa wanafunzi kwa ajili ya kuajiriwa kwenye uchumi rasmi.

Mwaka 2014 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ilizindua Sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya mwaka 2014 ambayo ina lengo la kuinua ubora wa elimu kupitia hatua kadhaa. Hatua hizo ni pamoja na kuboresha ufuatiliaji, kurekebisha mitaala ili kuifanya elimu ishabihiane na mahitaji ya jamii pia iendane na mbinu za kisasa za ufundishaji na ujifunzaji wenye ufanisi zaidi, kuboresha huduma za msingi kwa watoto shuleni, miundombinu ya shule na kujenga mazingira salama kwa watoto wote.

1.5 Juhudi za Serikali na Mafanikio

Tanzania imedhamiria kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo mwaka 2025 na imeandaa miongozo kadhaa ya kisera ili kutekeleza azma hii. Baadhi ya mafanikio makubwa hadi sasa ni haya:

1.5.1. Uandikishaji Umeongezeka maradufu

Mafanikio makubwa yamepatikana kwenye kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa shule ndani ya kipindi cha miaka 10 iliyopita. Ushahidi unaonesha kuwa uandikishaji umepanda kwa asilimia 26 kwa shule za msingi na sekondari. Ongezeko kubwa zaidi limeshuhudiwa kwenye uandikishaji wa wanafunzi sekondari kwa asilimia 244 na udahili elimu ya juu kwa asilimia 438.

1.5.2. Ugharamiaji wa elimu

Mwenendo wa hivi karibuni wa bajeti ya elimu unaonesha kuwa bajeti ya elimu ya Tanzania imeendelea kubaki kiwango cha 21% ya bajeti ya taifa. Hata hivyo, mgawo wa sekta ya elimu kwenye bajeti ikiwa ni pamoja na kulipa madeni ya taifa imebakia katika wastani 17%, ikimaanisha kuwa kwa miaka kadhaa hakujawa na ongezeko kwenye eneo hili ikilinganishwa na bajeti ya taifa.

1.5.3. Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014

Kupitia Sera hii ya elimu ya 2014, Serikali imedhamiria: kutoa ElimuMsingi bila ada, kuinua ubora wa elimu kwa kuimarisha udhibiti ubora na ukaguzi wa shule, kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kama vile miundombinu ya shule, kutoa vifaa vya kujifunzia kwa usawa, na kuboresha utendaji wa walimu kwa kutoa mafunzo ya ualimu kazini na motisha. Hata hivyo, ili kufanikisha haya yote, serikali inahitaji kuongeza mgawo na upelekaji wa fedha pamoja na kusimamia kikamilifu utekelezaji na matumizi ya fedha zilizotengwa.

1.6 Changamoto za Elimu

Licha ya juhudi za serikali zinazoendelea, sekta ya elimu nchini Tanzania bado ni imesongwa na changamoto nyingi. Baadhi ya changamoto kubwa ni hizi zifuatazo:

- Matokeo duni ya ujifunzaji kwa wanafunzi,
- Utoro wa walimu na umahiri duni wa kufundisha,
- Kukosekana kwa usawa wa kijinsia,
- Kutojumuishwa kwa watoto wenye mahitaji maalum na mazingira magum,
- Ukatili uliokithiri mashuleni
- Kushamiri kwa mfumo-tabaka wa elimu ambapo wenye pesa wachache wanamudu elimu bora kwenye shule binafsi na maskini wanaachwa kwenye elimu duni shule za serikali
- Kukosekana kwa falsafa na malengo ya elimu vinavyoeleweka kwa kila mtu. Matokeo yake, elimu ya Tanzania imekosa falsafa na malengo ya kuiongoza.





2.0

TUNATAKA KUFANYA NINI: MAENEO TUNAYOLENGA KATIKA MPANGO MKAKATI 2017-2021

2.1 Kushawishi mabadiliko ya sera na utekelezaji wake

Elimu ya Tanzania haina falsafa iliyo wazi na inashindwa kufikia ujumuishaji kamili wa makundi yote, imeshindwa kutoa matokeo bora ya kujifunza na yenye manufaa kwa wanafunzi. Wasichana bado ni waathirika zaidi. Shule si sehemu salama, kwani mtoto mmoja kati ya wawili hukumbana na ukatili, ambao umezoeleka kutendwa na walimu kuna haja ya kufanyia marekebisho zaidi sera ya elimu na kampeni ya kuhimiza utekelezaji makini wa sera ya elimu ya mwaka 2014 ili kuhakikisha upatikanaji wa elimu na ubora wake vinaimarika. Hata hivyo, kushughulikia ukatili, kutengwa na kubaguliwa baadhi ya watoto na masuala mengine kunahitaji mbinu na jitihada za pamoja kwa wadau mbalimbali na kuendelea kuutaarifu umma na kuhimiza mijadala ya umma.

Katika kipindi cha miaka mitano ijayo, lengo kuu litakuwa kufanya ushawishi kwa Serikali ili iandae na kutekeleza sera zinazozingatia ushahidi ambazo zitakuza fursa za watoto kuandikishwa shule, usawa na elimu jumuishi iliyo bora na inayotolewa kwenye mazingira rafiki na salama kwa wote.

Mwisho wa siku, tunataka kuwa na mfumo wa elimu ulioboreshwa ambao unahimiza usawa, ujumuishaji na ujifunzaji wenye ufanisi. Huu utakuwa mfumo ambao unahimiza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia na kukuza usawa wa jinsia, na mazingira rafiki ya kufundishia na kujifunzia; sera na mikakati ya elimu inatekelezwa kwa ufanisi na mapungufu yaliyoainishwa kwenye sera ya elimu ya mwaka 2014 yanashughulikiwa, na falsafa ya elimu Tanzania na masuala mengine muhimu ya kisera yanajadiliwa na mapendekezo yanatolewa.

Lengo la 1: Kufanya ushawishi kwa Serikali ili itunge na kutekeleza sera zinazozingatia ushahidi ambazo zitakuza fursa za watoto kuandikishwa shule, usawa na elimu jumuishi iliyo bora na inayotolewa kwenye mazingira rafiki na salama kwa wote.		
Matokeo: Mfumo wa elimu ulioboreshwa ambao unahimiza na kukuza usawa, ujumuishaji na ujifunzaji wenye ufanisi		
Matokeo tarajiwa		
Tarajio 1: Mazingira yanayokuza ufundishaji na ujifunzaji unaozingatia usawa wa jinsia, na kuweka mazingira rafiki na salama kwa wote yanaimarishwa	**Tarajio 2:** Sera na mikakati ya elimu inatekelezwa kwa ufanisi na mapungufu yaliyoainishwa kwenye sera ya elimu ya mwaka 2014 yanashughulikiwa	**Tarajio 3:** Falsafa ya elimu Tanzania na masuala mengine muhimu ya kisera yanajadiliwa na mapendekezo yanatolewa



2.2 Kukuza ushiriki wa wananchi na kujishughulisha

Kiwango cha ushiriki wa wananchi katika sekta mbalimbali za kiutawala nchini Tanzania, na hasa kwa wanawake, kiko chini sana na bado kinashuka. Kwa mfano, ushiriki wa wananchi katika vikao vya kamati za shule ulipungua kutoka asilimia 36 mwaka 2006 hadi kufikia asilimia 15 mwaka 2013, hii ni sawa asilimia 13 ya kushuka kwa ushiriki wa wananchi kwenye huduma hii muhimu ya umma.

Ni asilimia 22 tu ya wananchi, hasa wanaume, huhudhuria mikutano ya mabaraza ya vijiji ambayo ni fursa muhimu kwa ajili ya kujadili masuala muhimu ya kijiji na kufanya maamuzi yanayoathiri watoto na elimu. Na ni asilimia 16 tu ya wananchi ndio hushiriki katika kuandaa mipango ya kata na ya vijiji. Idadi kubwa ya washiriki hawa ni wale waliopata elimu ya msingi tu, hii ina maana kuwa wasomi wengi kwa kiasi kikubwa hawashiriki michakato hii muhimu.

Matokeo yake ni kwamba, ingawa kamati za shule,



mikutano ya vijiji na kata ni fursa muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi yanayoathiri watoto na elimu, kwa viwango hivi vidogo vya ushiriki wa wananchi, kuna uwezekano changamoto za sekta zitaendelea kubaki bila kutatuliwa.

Ndiyo maana Mkakati huu unataka kuhakikisha kuwa wananchi wanapata taarifa, wanajipanga na kushiriki kutatua matatizo muhimu, kufuatilia utawala na utoaji wa elimu bora. Tutajitahidi kufanikisha hili kwa kuhakikisha kuwa tunakuza na kuimarisha uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya elimu pamoja na masuala ya jinsia na ukatili dhidi ya watoto; tutahakikisha ushiriki wa wananchi na ufuatiliaji wa utawala wa shule na utoaji wa elimu bora unaboreshwa, na kwamba tutatafsiri na kuchapisha kwa lugha rahisi na kusambaza Sera, Sheria, Nyaraka na Miongozo ili kuwawezesha wananchi kuichambua na kuitekeleza kwa ufanisi.

Lengo la 2: Kukuza ushiriki wa wananchi kwenye utoaji na ufuatiliaji wa usawa, ujumuishwaji na ubora wa elimu		
Matokeo: Wananchi wanapata taarifa, wanajipanga na kushiriki kutatua matatizo muhimu, kufuatilia utawala na utoaji wa elimu bora		
Matokeo tarajiwa		
Tarajio 1: Uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya elimu jinsia na ukatili dhidi ya watoto unaimarishwa	Tarajio 2: Ushiriki wa wananchi na ufuatiliaji wa utawala wa shule na utoaji wa elimu bora ni unaboreshwa	Tarajio 3: Sera, nyaraka na miongozo itatafsiriwa, kuchapishwa kwa lugha rahisi ili kuwawezesha wananchi kuitekeleza kwa ufanisi.



2.3 Kukuza uwazi na uwajibikaji

Uwazi na uwajibikaji ni mambo muhimu kwenye utawala wa kidemokrasia. Kwa sababu, Uwazi wa serikali unawawezesha walipakodi, kutafiti na kujua kiurahisi utendaji wa serikali na kuiwajibisha serikali au viongozi wa kuchaguliwa kutokana na jinsi wanavyotumia fedha za walipakodi kwenye ngazi zote za serikali. Uwazi wa serikali unamaanisha kuweka taarifa zote za kifedha na taarifa za umma kuwa wazi kwa wananchi, rahisi-kwa-matumizi, katika mifumo iliyo rahisi kueleweka. Hii inawapa fursa walipakodi kuona waziwazi jinsi watumishi wa umma wanavyotumia fedha za kodi, na inawapa uwezo wananchi wa kuwawajibisha viongozi wao wa kuchaguliwa. Serikali yenye uwazi ni muhimu kwa ushiriki wa wananchi walio na taarifa, na wananchi waliohabarika ni muhimu sana kwa demokrasia.

Uwajibikaji hubeba kiwango ambacho mamlaka kama vile mamlaka za serikali za mitaa zinapaswa kuelezea au kuhalalisha kile walichofanya au walichoshindwa kufanya.

Kwa bahati mbaya nchini Tanzania, kiwango cha uwazi wa bajeti ya serikali kiko chini ya kiwango kinachotakiwa kimataifa. Hii inazuia ushiriki wa umma kwenye michakato ya bajeti na inaweka matatizo makubwa kwenye ufuatiliaji wa matumizi ya fedha katika utoaji wa huduma za kijamii na uwajibikaji kwenye fedha za serikali. Kwahiyo, HakiElimu itaendesha kampeni ya kudai uwazi zaidi na uwajibikaji kwenye matumizi ya rasilimali za umma ili kujenga mfumo wa utoaji huduma za umma wenye ufanisi.

Lengo la 3: Kukuza na kutetea kuwepo kwa uwazi zaidi na uwajibikaji kwenye utoaji elimu bora	
Matokeo: Serikali na wadau wanakuwa wasikivu na wanawajibika kutoa elimu jumuishi na bora	
Matokeo tarajiwa	
Tarajio 1: Mahitaji na madai ya wananchi kwenye elimu yanatetewa	**Tarajio 2:** Uwazi na uwajibikaji wa serikali na shule unakuzwa



3.0

TUNAFANYAJE KAZI?



Ili kufanikisha malengo haya, HakiElimu itaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na washirika wa ndani na wa kimataifa.


Hapa nchini, Shirika letu litaendelea kufanya kazi kwa karibu sana na mashirika yenye nia na malengo yanayofanana na HakiElimu kama vile Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Policy Forum na mengineyo. Tutaendelea pia kufanya kazi nchi nzima kupitia Marafiki Elimu (Mtandao wa watu binafsi, taasisi na vikundi) kuongoza juhudi za kuwahamasisha watu kushiriki kikamilifu kwenye usimamizi na ufuatiliaji wa utendaji kwenye elimu katika maeneo yao. *Marafiki wa Elimu* wanafanya kazi kama mawakala wa mabadiliko kwenye elimu wakiongoza, kushawishi na kuleta mageuzi na demokrasia kwa kuhamasisha wananchi wa kawaida kushiriki kutoa maamuzi, kufuatilia sera na utendaji wa serikali na mijadala ya umma. Hadi mwaka 2016, harakati za *Marafiki wa Elimu* zimefikisha idadi ya wanachama 40,000 Tanzania nzima ambao ni - watu binafsi, taasisi na vikundi.

Katika nyanja ya kimataifa, mkakati mpya wa HakiElimu umefungamana moja kwa moja na Malengo ya Maendeleo Endelevu namba 4[1] na 5[2] na kazi zetu zimeendelea kutambuliwa na kukubalika

kwa jumuiya ya wafadhili wa kimataifa wenye nia na malengo yanayofafana na yetu kama vile Shirika la TanFiDe, IBP, ADD, n.k. HakiElimu itaendelea kuimarisha mahusiano haya kupitia kanuni za ubia, kuheshimiana na uwazi.

1 SDG 4: Kuhakikisha elimu jumuishi, yenye usawa na ubora inatolewa na kukuza fursa za kuendelea kujifunza kwa wote
2 SDG 5: Kufikia usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake na wasichana wote

NADHARIA YA MABADILIKO YA MPANGO MKAKATI WA HAKIELIMU 2017 – 2021





Mawasiliano:

Kitalu Na. 739 Mtaa wa Mathuradas,
Mkabala na Barabara ya Umoja wa Mataifa
Upanga, Ilala, Dar es Salaam, Tanzania
Simu (Ofisi) : +255 (0) 22 2151852/3
+255 78 7655000 | +255 75 4354681
Nukushi: +255 (0) 22 2152449
Tovuti: http://hakielimu.org